**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUKAMATWA WAANDISHI WA HABARI, UVUNJIVU UHURU WA KUKUSANYIKA , KUTOA NA KUPOKEA HABARI KINYUME KATIBA YA TANZANIA NA SHERIA ZA NCHI**

**Februari 5, 2022**

Februari 3, 2022 walinzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ikishirikiana na polisi waliwakamata waandishi sita wa habari ndani ya Eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) Mkoani Arusha, Tanzania. Waandishi hao walikaguliwa, kuhojiwa na kunyanyaswa ikiwa ni pamoja na kudhihakiwa katika Lango la Lodoare.

Baada ya saa kadhaa waliachiwa kwa sharti la kuonana na Bajuta, mtumishi wa NCAA. Walikutana nae mjii Karatu usiku nae aliendelea kuwatishia kuhusu kuingia hifadhini bila kibali. Hata hivyo waandishi hao walifuata sheria zote ikiwa ni pamoja na kulipa kiingilio.

Waandishi waliokamatwa, na vyombo vyao kwenye mabano, ni Amina Ngahewa (Mwananchi Digital), Allen Isaack (Nipashe), Profit Mmanga (Wasafi TV), Apolo Benjamin (Daily News Digital), Janeth Mushi (Mwananchi) na Julius Sagati (Star TV).

Waandishi hao walienda kuripoti mkutano ulioandaliwa na wafugaji wa KiMaasai. Mkutano huo uliofanyika Kata ya Nainokanoka kupinga ukiukwaji wa haki za binadamu pamoja na mpango wa Serikali kuwahamisha kwa nguvu kutoka katika ardhi yao ya urithi.

Alfajiri siku ya mkutano huo askari wa NCAA pamoja na polisi walitanda katika uwanja ambao wafugaji walipanga kufanya mkutano wao wa Amani. Uwepo wa askari hao kwenye uwanja wa mkutano bila shaka ulilenga kuwatisha wafugaji hao kuhudhuria mkutano huo.

Tunalaani ukiukwaji huu wa haki ya habari kwani siyo tu ni unavunja katiba ya Tanzania, lakini Vile vile ni kunyume cha sheria za nchi na za kimataifa.

Hivyo tunalaani vitendo vya polisi na askari wa mamlaka kuingilia uhuru wa wafugaji kukusanyika. Tukio hili linakiuka haki ya Watanzania kukusanyika.

Tunalaani vitendo vya kuwatisha wananchi wa jamii ya kiMaasai kuhudhuria mkutano halali, na wa amani, na kuwakamata waandishi wa habari ni mkakati usiofaa wa taasisi husika za serikali

kuhakikisha kwamba umma hauelezezwi matatizo sugu ya ukiukwaji wa haki za binadamu wanayofanyiwa waMaasai wa Ngorongoro.

**Matatizo Sugu ya waMaasai Ngorongoro**

- Kukiuka lengo la kuanzishwa NCA kwa hasa lengo mahususi la "kulinda na kuendeleza maslahi ya waMaasai raia wa Tanzania wanaofuga ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro."
- Ongezeko la shughuli za kibinadamu ikiwa ni pamoja na hoteli na magari. Kuna hoteli lukuki Ngorongoro zilizojengwa kwenye maeneo tete ikiwemo Ukingo wa Kreta ya Ngorongoro. Zingine zimejengwa kwenye mapario ya wanyamapori na mifugo. Wakati kuna waMaasai chini ya 90,000 Ngorongoro watalii zaidi ya 700,000 hutembelea eneo hilo kila mwaka (kabla ya Uviko 19) wakitumia ndege na magari zenye kelele.
- NCAA kutowashirikisha wafugaji wenyeji wa NCA kwenye mipango ya usimamizi wa shughuli za uhifadhi.
- WaMaasai kudhibitiwa kwa matumaini kuwa ufukara utawalazimisha tu kuondoka.
- Kuwepo kwa ufukara na baa la njaa. Zaidi ya 50% ya waMaasai ni mafukara wakati 70% wanakabiliwa na janga njaa ya kudumu katika eneo linaloingiza fedha nyingi kutokana na utalii.
- Asilimia 64 ya WaMaasai Ngorongoro hawajui kusoma na kuandika sababu ya umasikini.
- Upotoshaji unaoendeshwa kwenye vyombo kuonyesha kuwa WaMaasai wanaharibu NCA.
- Tishio la kudumu la kuhamishwa kutoka kwenye ardhi yao kinyume na sheria.

**Ukweli kuhusu haki za waMaasai Ngorongoro**

Eneo la Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro ni ardhi inayomilikiwa kimila na wafugaji. Kuna vijiji 25 ndani ya eneo hilo ambavyo hadhi zao sio tofauti na vijiji vyote Tanzania.

Mwaka 1958 Serikali ya kikoloni ya Tanganyika iliwahamisha kimabavu waMaasai kupisha kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti yenye ukubwa wa 15,000 $km^2$.

WaMaasai walibakiwa na eneo dogo (8,100 $km^2$), la iliyokuwa ardhi yao, yaani NCA. Pamoja na hayo wafugaji hao wanatumia ardhi hiyo na wanyamapori na watalii.

Serikali iliahidi mwaka 1958 kuwa haitawahamisha tena waMaasai kutoka Ngorongoro.

**Mapendekezo**

- The NCAA Pamoja na vyombo vingine vya usalama vizingation haki za kujieleza haki za kujumuika na kutoa taarifa na uhuru wa jamii kujieleza na kutoa malalamiko
- NCAA isitishe maramoja unyayasaji na vitisho kwa viongzoi wa jamii, watetezi haki za binadamu na waandishi wa habari wakiwa katika shughuli zao zinazoruhusiwa kikatiba
- Tunaitake NCAA NCAA kusitisha propaganda zake ambazo sio za kweli kupitia vyombo vya Habari zenye lengo la kchafua na kuposha taswira ya jamii kwa nia ya jamii kuonekana kwamba ndio chanzo cha matatizo ya NCAA
- Serikali iunde tume huru itakayowahusisha wafugaji wenyeji wa Ngorongoro, wataalam wa uhifadhi, watetezi wa haki za binadamu, wadau wa utalii, wataalam wa mifugo, wadau wa haki za binadamu na kutafuta namna yenye kuzingatia haki kuiendeleza Ngorongoro.
- Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na NCAA ziachane na nia ovu ya kuwahamisha wafugaji kutoka Ngorongoro kusudi kulinda haki za wenyeji ambao hiyo ni ardhi yao.
- Serikali iendeleze mbinu endelevu za ufugaji ambazo ndiyo sababu kuna wanyamapori.
- Serikali ikomeshe tatizo sugu la njaa Ngorongoro kwa kuruhusu kilimo katika vijiji 25 na kuacha kukataza mifugo kula majani na kupata maji. Hizi ndizo sababu za njaa NCA.
- Serikali iunde kamati huru kuchunguza ukiunkwaji wa haki za binadamu kwa miongo 6.

Imetolewa na PINGOs Forum Leo tarehe 5/2/2022